# Tanzania yapata soko la maziwa Kenya

**Na Theopista Nsanzugwanko**

KAUNTI ya Migori nchini Kenya imekumbwa na uhaba mkubwa wa maziwa na kuagiza asilimia 10 ya mahitaji yao kutoka Tanzania.

Bodi ya Maziwa Tanzania imesema mahitaji hayo ni fursa kubwa ya biashara ya maziwa kwa Tanzania, hivyo imejipanga kuhakikisha yanauzwa kwa utaratibu rasmi kwa manufaa ya wananchi na nchi.

Mtendaji wa Kilimo katika kaunti hiyo, Valentine Ogongo alisema juzi kuwa uzalishaji wa maziwa katika eneo hilo haujafikia mahitaji na takwimu za Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi zinaonesha kuna uzalishaji wa lita milioni 25 za maziwa kwa mwaka ikiwa ni chini ya mahitaji ya lita milioni 88 kwa mwaka.

Kutokana na upungufu huo, kaunti hiyo imelazimika kuingiza takribani asilimia 10 za maziwa yanayohitajika kutoka Tanzania, huku asilimia 20 ya maziwa yake yakipatikana kutoka Trans Mara, Nandi na Homa Bay.

Ogongo alisema uhusiano mzuri kati ya Kenya na Tanzania umerahisisha kuingizwa kwa maziwa nchini humo.

"Tunategemea maziwa kutoka Trans Mara, Nandi na hata kutoka Tanzania. Wakulima wetu wana uwezo wa kupata maziwa kutoka nchi jirani kwa sababu ya uhusiano mzuri kati ya nchi hizi mbili; " alisema Ogongo.

Ongezeko la idadi ya watu, mabadiliko ya hali ya hewa, aina ya malisho wanayopatiwa ng'ombe yametajwa kama sababu zinazochangia upungufu wa maziwa katika kaunti hiyo.

Kutokana na uhaba huo, serikali ya kaunti hiyo imeshirikiana na Benki ya Dunia na wadau wengine kukuza uzalishaji wa maziwa.

Kaunti hiyo ilizindua mpango wa kutoa ng'ombe wa maziwa kwa wakulima wa miwa na tumbaku mwaka 2014, ambapo waliwekwa katika vikundi vya watu 10 na kupewa ng'ombe mmoja, huku wakulima wengine wakipewa ndama kama kianzio cha kufuga.

Akizungumzia biashara hiyo, Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Noel Byamungu alisema wanatafuta kwa kiasi kikubwa soko la nje la bidhaa hiyo lakini kwa utaratibu maalumu.

"Kwa sasa nchi haijaanza kusafirisha maziwa nje ya nchi lakini katika kaunti hiyo ambayo iko mpakani na inapakana na kabila moja la Tanzania inawezekana kufanyika kwa biashara hata hivyo siyo rasmi hivyo tunafuatilia ili kuanza kuuzwa rasmi," alisema.

Byamungu alisema hiyo ni fursa kubwa ya kuuza bidhaa hiyo nje hivyo ni lazima nchi kuwa na taarifa ya kiasi kinachouzwa na kutoa elimu kwa wananchi jinsi ya kufanya biashara na kupata vibali rasmi.

"Kuna maziwa mengi katika maeneo hayo na bodi ilikuwa ikishangaa yanaenda wapi, hii ni taarifa muhimu kwetu tutafuatilia ili kuweka utaratibu mzuri na kupata takwimu sahihi licha ya kuwa kutokana na ushindani wa kibiashara kwa maziwa inaweza kuwa changamoto," alisema.

Scanned with CamScanner

# Serikali kuwakomalia watakaojihusisha uvuvi haramu

**Na Fresha Kinasa, Mara**

SERIKALI Mkoa Mara imesema, itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa watu watakaobainika kujihusisha na vitendo vya uvuvi haramu ndani ya Ziwa Victoria.

Mbali na hilo, pia imewataka wananchi kutojihusisha na vitendo vya ujangili ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, ili kuhakikisha hifadhi hiyo inaendelea kutoa mchango wa kimaendeleo katika ukuaji wa uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa ambapo alisema jukumu la kulinda rasilimali za Ziwa Victoria pamoja na wanyama ndani ya Hifadhi ya Serengeti, linapaswa lifanywe na kila mmojaw ili kuhakikisha vizazi vijavyo vinanufaika na rasilimali hizo.

Alisema kutokana na juhudi kubwa zilizofanywa na serikali kupambana na uvuvi haramu, kumewezesha upatikanaji wa samaki wakubwa jambo ambalo awali haikuwezekana.

Malima alisema juhudi za kupambana kulinda rasilimali hiyo ndani ya ziwa, lazima iwe thabiti na kwamba mtu yeyote akibainika kujihusisha na uvuvi haramu, lazima achukuliwe hatua kali za kisheria bila kufumbiwa macho.

"Vitendo vya uvuvi haramu havipewi nafasi hata kidogo, tumeona ambavyo nguvu kubwa ya kupambana na uvuvi haramu ilivyoleta manufaa kwa sasa samaki wakubwa sato na sanagara, wanapatikana na bila juhudi hizo kufanyika ziwa lingebakia maji matupu.

"Niombe wananchi wote tushirikiane kwa pamoja kulitunza ziwa letu ili samaki, wazaliane kwa wingi na wavuliwe kwa utaratibu unaofaa, nikiwa Mkuu wa Mkoa, nitasimamia jambo hili kwa dhati," alisema.

Kuhusu vitendo vya ujangili katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Malima alisema serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuhakikisha hifadhi hiyo inakuwa salama.

Aliwataka wananchi waendelee kuwa walinzi na wasijihusishe na vitendo hivyo, lengo ni kuifanya hifadhi hiyo izidi kuwanufaisha Watanzania katika kuingiziza fedha za kigeni, ambazo zitachangia ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Katika hatua nyingine, Malima aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mara kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kutojihusisha na vitendo vya uvunjifu wa amani ikiwemo uhalifu.



Scanned with CamScanner

# Wafanyabiashara wa mifugo wanolewa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) juzi imeendelea na zoezi la utoaji mafunzo ya siku saba kuhusu upataji wa leseni ya biashara kwa njia ya mtandao kwa wafanyabiashara wa mifungo waliopo Pugu mnadani jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia juu ya dhumuni la mafunzo hayo, Afisa Biashara wa BRELA,Peter Riwa alisema, lengo la kuu la kushiriki katika mafunzo hayo ni kutoa elimu na hamasa kwa wafanyabishara.

"Dhumuni kuu ni kuwafikia wadau wetu na kuwapa elimu juu ya huduma tunazotoa, kuwahamasisha wadau juu ya leseni za biashara, kuwasogezea huduma karibu na kutatua changamoto za wadau wetu papo kwa hapo pindi wanapopatiwa elimu,"alisema.

"Aidha zoezi hili ni moja ya mkakati wa kuondoa na kupunguza urasimu wa uwepo wa watu wa kati (VISHOKA) wanaokwamisha taratibu za upatikanaji wa Leseni kwa wafanyabishara,"alieleza Riwa.

Naye Mkuu wa mnada, Kerambo Samwel alieleza baadhi ya changamoto wanazopitia lakini pia kupongeza juhudi za BRELA.

**INAENDELEA UK. 3**

Scanned with CamScanner

# Serikali yajikita kutatua changamoto za wafugaji

**Na Mbaraka Kambona, Mpwapwa**

KAIMU Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Dkt. Jonas Kizima amesema utafiti wanaoufanya umejikita katika kutatua changamoto za mbegu bora za mifugo na za malisho kwa wafugaji, ili sekta ya mifugo iweze kuchangia vyema pato la taifa.

Dkt. Kizima aliyasema hayo alipotembelea kukagua shughuli zinazofanywa na Kituo cha TALIRI Mpwapwa, kilichopo wilayani hapa mwishoni mwaka wiki.

Alisema lengo la utafiti wanaoufanya ni kuhakikisha wanapata mbegu bora za mifugo na kuzalisha mbegu bora za malisho ya mifugo, zitakazosaidia kutatua changamoto za upatikanaji wa mbegu bora za mifugo zinazohimili mazingira yaliyopo na malisho inayoikabili nchi kwa sasa.

Aliongeza kuwa kwa sasa taasisi hiyo, inaendelea na kufanya tathmini ya ubora, ustahimilivu na makuzi ya malisho ya mifugo, yatakayofaa kwa chakula cha kutosha kwa ajili ya mifugo.

Kwa mujibu wa Dkt. Kizima, matokeo yoyote ya utafiti lazima yabadilishwe kuwa biashara kwa sababu wafugaji wakifanya ufugaji unaoendana na mazingira yao, itawasaidia kutengeneza uchumi na kuwaongezea tija katika ufugaji wao.

"Tafiti tunazozifanya zinalenga kuimarisha mnyororo wa thamani wa mifugo, ili mchango wa sekta ya mifugo uweze kuonekana katika uchumi wa kati," alisema.

Dkt. Kizima alisema, TALIRI imesambaza vituo vyake katika kanda saba nchini ili kuwa karibu na wafugaji kuwasaidia kutatua changamoto zao kwa ajili waweze kufanya ufugaji wenye tija.

Alisema vituo hivyo vipo katika Kanda ya Mashariki, Kaskazini, Kati, Kusini, Magharibi, Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini.

Naye Mkurugenzi Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani, Dkt. Angello Mwilawa alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi imezihamasisha halmashauri zote nchini, kuanzisha mashamba darasa ya malisho ili wafugaji waweze kujifunza na kupata mbegu bora za malisho kwa ajili ya mifugo.

"Tunawahimiza wafugaji kuona umuhimu wa kulima malisho, ili yaweze kuwasaidia kupata lishe ya uhakika kwa mifugo yao na pia kwa kulima malisho kutawapunguzia migogoro ya mara kwa mara kati yao na wakulima," alisema.

Aliongeza kuwa, wanawahamasisha wafugaji hususan walio katika nyanda kame wastawishe malisho ya mifugo wakati wa masika na kuyatunza, ili yaweze kuwasaidia kulisha mifugo yao wakati wa kiangazi.



**Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Huduma za Ugani, Dkt. Angello Mwilawa akiwaeleza waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu utafiti wa malisho unaofanywa na Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Mpwapwa, alipotembelea moja ya shamba la malisho ya mifugo la kituo hicho mwishoni mwa wiki. Kulia kwake ni Kaimu Mkurugenzi Msaidizi, Utafiti na Mafunzo, Dkt. Hassan Mruttu.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner